COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD

Tuesday, 7th May, 2024

Third Assembly – Third Session
THIRTY SECOND SITTING

[The County Assembly met at 2:46p.m. at the County Assembly Buildings]
[The Temporary Speaker (Honourable Frankline Makanga) in the Chair]

PRAYERS

The Temporary Speaker (Hon. Makanga)**:** Tunaweza kuketi Waheshimiwa. Ahsante Waheshimiwa, labda Katibu uweze kutujulisha kama tuko na takwimu za kutosha za kuendeleza kikao hiki.

[Lack of quorum]

Kulingana na Kanuni zetu za kudumu 31 (2) inaelezea yale yanayo paswa kufanywa endapo hakuna idadi ya Wajumbe ya kutosha katika Bunge inapoanza vikao vyake na imetuamuru kwamba endapo hilo litafanyika, basi Mwenyekiti aamrishe kengele kupigwa kwa dakika zengine kumi ili kuona kama tutapata idadi ya Waheshimiwa ama Wajumbe wawakilishi. Kwa hivyo naamrisha kwamba kengele hiyo iweze kupigwa kwa dakika kumi ili tuone kama tutapata idadi hiyo. Ahsante…

[The Serjeant-At-Arms rung the quorum Bell]

Please Clerk you confirm for us if we now have Quorum?

[Lack of quorum]

Mheshimiwa Katibu, Bwana Katibu naona hesabu inasema ni saba badala ya sita. Kulingana na Kanuni hizo za Kudumu zinasema ya kwamba, endapo baada ya dakika kumi idadi bado itakuwa haijatoshea, kengele ipigwe tena kwa dakika tano. Tafadhali kengele hiyo ipigwe tena kwa dakika tano.

[The Serjeant-At-Arms rung the quorum Bell]
[Loud Consultations]

Naam Katibu, tujulishe kama tuko na idadi ya kutosha.

[Lack of quorum]

Ahsante Mheshimiwa Katibu. Mheshimiwa Milka sijui mazungumzo yako yataongezea idadi ya Waheshimiwa ama?

Hon. Ngare: Najaribu kumpa mawazo ndio kesho tunaweza kufanya kitu.

The Temporary Speaker (Hon. Makanga)**:** Mheshimiwa Milka, hayo unayoyasema ni mawazo yako ambayo hayafai kuwa katika Rekodi za Bunge hili ni kweli ama uongo?

Hon. Ngare: Ni kweli.

The Temporary Speaker (Hon. Makanga)**:** Kulingana na Kanuni za kudumu za Bunge hili 31(1) na (2) inasema kwamba endapo hatutakuwa na idadi ya kutosha katika Bunge, Bunge linapoanza kikao chake na baada ya kupiga kengele kwa dakika kumi na dakika tano mtawalia na idadi hiyo ikose kuafikiwa, basi Bunge litaahirishwa hadi kikao kilicho mbele yake. Kulingana na kanuni hizo na sheria zetu, Bunge hili limeahirishwa hadi tarehe nane saa nne asubuhi. Shukran.

The House rose at 2:59p.m.